Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Australia

Toleo: 03 / 1446 H

Jumatatu, 30 Muharram 1446 H

05/08/2024 M


## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

# Kama Umma Mmoja: Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa Kuangamizwa kwa Dhalimu Hasina na Tunawaombea Kuporomoka Madhalimu Wote Wanaoukandamiza Ummah

**(Imetafsiriwa)**

Baada ya majuma kadhaa ya ukandamizaji wa kikatili dhidi ya watu wa Bangladesh na dhalimu Hasina, genge la serikali yake, na wachungaji wake wa kigeni, alilazimishwa kidhalilifu kuikimbia nchi. Waislamu shupavu wa Bangladesh, wakiongozwa na wanafunzi jasiri, walivumilia ukatili usio na kifani na hatimaye kulazimisha kuondolewa kwake kupitia wimbi lisilozuilika la maandamano ambayo yalimshinda dikteta huyo.

Waislamu wa Bangladesh kwa mara nyingine tena wameangazia uwezo mkubwa ndani ya ummah, wakionyesha hatima isiyoepukika inayowangojea madhalimu wanaowafanyia ukatili raia wao. Ingawa huu ni ushindi wa aina yake, ummah lazima uzingatie mafunzo ya matukio kama hayo katika nchi kama Misri na Sudan. Misimamo ya kikoloni inaenea ndani kabisa ya rasilimali za ummah, ikinyakua kwa ujanja ushindi kwa kuwatupilia mbali madhalimu vibaraka wao pindi kufaa kwao kunapokwisha, ila kuwabadilisha tu kwa watu ambao uaminifu wao unabakia mapajani mwa dola za kigeni na zenye uadui.

Umma lazima uhakikishe kwamba rasilimali zake, kama vile majeshi, zinabakia chini ya udhibiti wake ili kwamba matakwa ya uadilifu wa kweli kwa wote—yanayojumuishwa tu ndani ya mfumo ulioteremshwa na Mwenyezi Mungu (swt)—yaweze kuasisiwa kwa uhuru kamili na umma wa Muhammad (saw).

Tunawapongeza Waislamu wa Bangladesh kwa subira na ustahimilivu wao, na tunaomba dua kwamba Mwenyezi Mungu (swt) awakubali mashahidi wengi na huu uwe ndio mwanzo wa mwamko mkubwa kwa Waislamu wa Bangladesh katika kusimamisha rehma na uadilifu wa Uislamu kwa watu wote.

[وَلاَ تَحْسَبَنَّ اللهَ غَافِلاً عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الأَبْصَارُ]

***"Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatapo kodoka macho yao."*** *[Quran 14:42]*

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**Australia**


Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:
www.hizb-ut-tahrir.org

Tovuti: www.hizb-ut-tahrir.dk

Pepe: info@hizb-ut-tahrir.dk

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:
www.hizb-ut-tahrir.info